# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

## GRADE NINE 2026

GOLDEN MERIT

### KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

[9]

JINA: ............................................................

SHULE: ............................................................

NAMBARI YA MWANAFUNZI: ............................................................

**MAELEZO KWA MTAHINIWA**

(i). Andika jina lako na Nambari ya mtihani (ii). Jibu maswali yote kwenye karatasi hii.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI MUDA : SAA 1 DAKIKA 40

| | JUMLA YA ALAMA | ALAMA YA MTAHINIWA |
|---|---|---|
| | ALAMA 50 | |
| | | |

*Soma se* ... 0

SHULE YA MSINGI YA KIBOKO,
SANDUKU LA POSTA 101,
THIKA.
-2014.

Kwa binamu mpenzi,

Nakutumia salamu nikitumaini kuwa watu wote nyumbani hawajambo. Ndugu zangu na wazazi ni wazima na wameniambia niwapasie salamu zao. Safari yetu kutoka likizoni Mombasa ilikuwa nzuri, ijapokuwa gari letu lilitusumbua kidogo.

Tuliondoka Mombasa saa nne za mchana. Tulifika Mombasa saa nane za mchana. Tulipofika Voi, tuliteremka kunywa soda. Tuliporudi, gari lilikakataa kuwaka na tulilazimika kulisukuma. Sisi watatu, mimi, mama na kaka ndio tuliokuwa tukilisukuma na baba ndiye aliyekuwa ameshika usukani. Tulichoka sana. Lakini hatimaye tukafaulu na safari ikaanza tena. Tukafika nyumbani saa tano za usiku. Kama nilivyokueleza, likizo yetu mjini Mombasa ilikuwa ya kufana sana. Tulitembelea sehemu nyingi sana kama vile ngomeni,bandari ya kilindini, feri ya Likoni, ikulu ya Mombasa na kadhalika.

Sehemu hizo zote zilinivutia sana, hasa bandari ya kilindini. Niliweza kuziona meli kubwa za kubeba shehena na za abiria. Nilitaka sana kuzitazama ndani zilivyo lakini askari wa forodhani hawakunipa ruhusa. Haidhuru, nitapata nafasi siku nyingine. Tulipoitembelea soko ya Mombasa, niliweza kuona mapakacha ya matunda aina mbalimbali, vichala vya nazi, vikonyo vya saibibu, mananasi, mikungu ya ndizi na kadhalika. Gari letu halikuweza kubeba vitu mingi. Lakini tulinunua pakacha la matunda na nazi mbili, tu hivi. Nitakuwekea nazi moja kama nilivyokuahidi. Ni hayo tu sasa. Wape binamu wenzako na wazazi salamu zetu.

Ndimi wako mpenzi,
Sara Bakari.

1. Barua hii inaenda kwa____
   A. Binamu yake sara
   B. Mchumbake Sara
   C. Sara, kwenda kwa binamu yake
   D. Sara Bakari

2. Safari yao ya kurudi kutoka likizoni Mombasa ilianza _____
   A. saa moja darasani B. Saa nne mchana
   C. saa nane usiku D. saa tano za usiku

3. Waliokuweko katika safari hii walikuwa ni watu
   A. watatu B. wanne
   C. watano D. wawili

4. Mwandishi wa barua hii hakupata nafasi ya kuitazama meli ndani kwa kuwa ____

A. wenyewe hawakumpa ruhusa

B. askari wa bandari walimkataza

C. askari polisi walimkataza

D. atapata nafasi siku nyingine

5. Maana ya "ameshika usukani" ni ____

A. Analiendesha gari

B. analisukuma gari

C. anakaa bure kitini akicheza na kifaa cha kuliendesha gari

D. usukani umemshika

6. Neno lingine lenye maana na kufana ni ___

A. kucheza B. kupendeza

C. kuchukiza D. kufanana

7. Askari wa forodha hufanya kazi ya _

A. kutoza kodi ya bidhaa zinazoingia au kutoka nchini

B. kuwakataza watu wasilipe kodi

C. kuwakataza watoto wasiende karibu na meli

D. kupiga watu risasi

8. Chagua kinyume cha neno hili lililopigwa mstari:-

Wapiga mbizi walizama majini jana

A. waliyaibuwa B. walilipuka

C. waliibuka D. walijibwaga

9. Kijana huyo alieleza kisa chote ______ bila kuficha kitu.

A. kinaga ubaga B. ovyo

C. ghafula D. kamwe

10. Ni neno gani limesimamia yale mengine katika haya:

A. almasi B. shaba

C. madini D. dhahabu

Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 11hadi 17 kwa kila nafasi umepewa maneno hapo chini, chagua neno lifaalo zaidi kati ya hayo uliyopewa

Inaonekana kwamba vijana____11____ wa siku hizi wanapenda mambo ya starehe na anasa nyingi. Utawaona wengine wakinunua vitu vingi ____12____ bei ya juu kama vile televisheni za rangi na tepu za thamani kubwa.Mimi sipingi vijana kufanya vile wanavyopenda kwani wako katika ulimwengu wa ____13____.

Lakini ni jambo la kusikitisha sana kuona baadhi ya wazazi wa hawa watoto ____14____ wanaishi mashambani hawana chochote,wazazi hawana mavazi mazuri, hawapati chakula cha ____15____miili na nyumba ____16____ vile vile ni mbovu. Wanapotafuta misaada kwa watoto wao, husumbuliwa na kudanganywa huku watoto wao waliolemisha kwa taabu na ____17__ wanaponda mali sehemu za mijini..

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | vyetu | zetu | chetu | wetu |
| 2. | vya | viyaa | za | cha |
| 3. | kisa | kisasa | kichana | kisha |
| | ambayo | ambawo | ambao | ambaye |
| | kujenga | manufaa | kushiba | kunenepa |
| | wanavyokaa | wanayokaa | wanakaa | wanamokaa |
| | furaha | kicheko | mali | mashaka |

Maana ya usemi "alitokwa na maneno mengi yasiyo na maana" ni

A. aliropokwa B. aliteta

C. alilalamika D. aling'unika

Huku __________ ninakoishi

A. ndimo B. ndiyo

C. ndiko D. ndipo

20. Kamilisha methali hii:____ maji ukiyavulia nguo

A. Yamwage

B. Yachemshe

C. Yaogee

D. Usiyaguse

Kutoka swali 21-22 kwa kila methali ni maana yapi yaliyo kamili miongoni mwa . B, C, D

21. Usipoziba ufa utajenga ukuta
A. Ufa mdogo unaweza kuangusha nyumba
B. Ukuta huanguka baada ya kufanywa ufa
C. Usiporekebisha kosa ndogo unaweza kuleta hasara kubwa baadaye
D. Kila kosa dogo lazima huleta uzuri baadaye

22. Mchimba kisima huingia mwenyewe
A. Mwenye kufanyia watu jambo nzuri hupata yeye faida kubwa
B. Mwenye kuchimba kisima lazima aingie ndani kuchimbua
C. Mwenye kuwafanyia watu mambo mabaya hasara humfikia mwenyewe
D. Kila kisima kilichochimbwa kina mwenyewe

Kamilisha sentensi zifuatazo

23. Ungekula kidogo _________ njaa
A. ungelisikia B. ungeshiba
C. usingalisikia D. ungesikia

24. Usingalikuwa mwivi _____ mashaka
A. hawangekutilia B. hawangemtilia
C. hawangekutilia D. hangemtilia

Chagua neno ambalo halina uhusiano

25. A. Hayati B. Harakati
C. Marehemu D. Mfu

26. A. kinaganaga B. kikongwe
C. kibogoyo D. kilembwe

27. Babake babako utamwitaje?
A. baba B. mjomba
C. binamu D. babu

28. Ni nini udogo wa "Jipanga hili linakata?"
A. Kajipanga hiki kanakata
B. Kapanga haka kanakata
C. Kijipanga hiki kinakata
D. Kijipanga hiki kanakata

29. Mtoto alianguka "chumbwi" maana yake ni kuwa alianguka __
A. sakafuni B. matopeni
C. majini D. mchangani

30. Kinyume cha fumba ni ____
A. fumbata B. fungua C. funguo D. fumbua

31. Mtoto wa bata anaitwaje?
A. Shibli B. Kiyoyo C. Kivinimbi D. Kitungule

32. Ugonjwa wa kuhara na kutapika huitwa __________
A. homa B. waba C. mafua D. kifuakikuu

33. Ni nomino gani itaundwa kutokana na kitenzi fuga?
A. Kufuga B. Fungo C. Kufunga D. Mifugo

34. Moja kwa saba pia huitwa _______________
A. Subui B. Humusi C. Tusui D. Sudusi

35. Andika wingi wa sentensi hii .
Ami ni seremala hodari wa kutengeneza meza.
A. Ami ni seremala hodari wa kutengeneza mameza.
B. Akina ami ni seremala hodari wa kutengeneza meza.
C. Waami ni maseremala hodari wa kutengeza meza.
D. Akina ami ni maseremala hodari wa kutengeneza meza.

36. Tukisema kuwa baba ni simba hiyo ni tamathali gani ya lugha?
A. Tashbihi B. Methali C. Istiara D. Semi

37. Ni sentensi gani iliyo kwa wakati kamilifu au timilifu?
A. Mama amepika sima.
B. Mama alipika sima.
C. Mama atapika sima.
D. Mama anapika sima.

38. Anayeuza bidhaa kwa kutembezatembeza ni _______
A. mchuzi B. mjusi C. mchuuzi D. mjuzi

39. Neno kiwete limo katika ngeli gani?
A. KI – VI B. U – I C. U – U D. A – WA

40. Kanusha sentensi hii
Nikifanya bidii nitafaulu _______________
A. Sitafanya bidii wala sitafaulu.
B. Nisipofanya bidii sitafaulu.
C. Sikufanya bidii wala sikufaulu.
D. Sijafanya bidii na sijafaulu.

Soma habari kisha ujibu maswali 41 - 50.

Majambazi watatu jana waliuawa katika mtaa wa sokomoko, na wananchi waliokuwa wamepandwa na mori. Majambazi hao walikuwa miongoni mwa genge la majambazi lililovamia duka la mzee mlachake. Ilisemekana kuwa walimwiibia shilingi elfu mia mbili. Jirani yake kichwamaji na wengine walipiga mayowe baada ya majambazi hao kutoroka. Pia walipiga ripoti katika kituo cha polisi kupitia kwa mawasiliano ya rununu.

Mbiu ya mgambo ikilia ..... watu hao walikusanyika haraka na kuwavamia wezi hao kabla ya kutoroka. Wezi wawili walifua dafu kutoroka. Ilipatikana kuwa majambazi walikuwa na visu vikali, bunduki na rungu. Njenje walizoziiba zilipatikana katika mkoba waliokuwa nao.

Polisi walifika mahali hapo muda mfupi baadaye na kuwachukua wafu ufuoni na kumrudishia mzee pesa zake. Waliahidi kuwasaka wahalifu waliosalia.

41. Idadi ya wezi waliokuja kuiba ilikuwa ngapi?
   A. Watatu
   B. Wawili
   C. Watano
   D. Mia mbili

42. Wananchi waliopandwa na mori ina maana gani?
   A. Walivamiwa na mori.
   B. Walipata hasara.
   C. Kuwa na hasira.
   D. Waliogopa sana.

43. Tunasema genge la majambazi na _______________ cha askari.
   A. umati
   B. kilinge
   C. kicha
   D. kikosi

44. Pesa walizoiba ni ngapi?
   A. 20,000
   B. Laki mbili
   C. 200
   D. 2,000

45. Kamilisha methali hii.
   Mbiu ya mgambo ikilia _______________
   A. Funika kombe apite.
   B. Msema kesho ni mwongo.
   C. Kuna jambo.
   D. Tembo hulitia maji.

46. Maana ya kufua dafu ni _______________
   A. kosa kupata
   B. osha mahali
   C. toroka kwa kasi
   D. fanikiwa

47. Polisi walipashwaje habari?
   A. Wananchi walikimbia mpaka kituoni kuripoti.
   B. Walipigiwa simu.
   C. Walisikia mayowe.
   D. Walikuwa wameshika doria wakawapata.

48. Ni silaha gani ambayo majambazi hawakuwa nayo?
   A. Mkoba
   B. Risasi
   C. Bunduki
   D. Visu vikali

49. Ni sentensi gani isiyo kweli kulingana na habari?
   A. Wananchi waliua majambazi.
   B. Mzee mlachake alirundishiwa pesa zake zote.
   C. Si wezi wote waliuawa.
   D. Polisi waliua majambazi.

50. Kichwa mwafaka cha habari hii ni _______________
   A. mzee mlachake.
   B. polisi waua wezi.
   C. uhalifu haufai.
   D. heri uibe bora usishikwe.